

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



MKOA WA IRINGA  
Mkoa

Simu Na. 2702191  
Fax.Na.2702082  
Barua pepe: ras@iringa.go.tz

Ofisi ya Mkuu wa  
S.L.P. 858,  
**IRINGA.**

**Unapojibu tafadhali taja:**

Kumb.Na. RAS/003/2022-2023/W/02

6 April, 2023

## **TANGAZO**

### **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI KWA MAFUNDI KATIKA NYANJA YA UJENZI.**

<b>Na.</b>	<b>MAELEZO</b>	<b>NAMBAYA ZABUNI</b>
1.	Ujenzi wa Servant Quarter Katika Nyumba ya Makazi ya Katibu Tawala	RAS/003/2022-2023/W/02 lot 01
2.	Ujenzi wa "Hard Landscaping" katika nyumba ya Makazi ya Katibu Tawala	RAS/003/2021-2022/W/02 lot 02
3.	Ujenzi wa "Soft Landscaping" katika nyumba ya Makazi ya Katibu Tawala Mkoa.	RAS/003/2021-2022/W/02 lot 3

- i. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/2023 Ofisi ya Mkuu wa Mkoa iliidhinishiwa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi kama ilivyooneshwa katika jedwali hapo juu.
- ii. Utekelezaji wa miradi hiyo utafanyika kwa njia ya '**FORCE ACCOUNT**'.
- iii. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa inatarajia kuanza kutekeleza kazi hizo mara baada ya kupatikana kwa mafundi/wajenzi.
- iv. Katibu Tawala Mkoa anakaribisha maombi kutoka kwa mafundi/wajenzi vikundi, Taasisi za Umma na Taasisi Binafsi zenye nia na uwezo wa kutekeleza kazi hizo kwa ubora na viwango vinavyokubalika.
- v. Waombaji wote wenye nia ya kushiriki katika mchakato huo wanatakiwa kuwasilisha gharama za ufundi wa ujenzi wa nyumba za makazi na Ofisi kama ilivyofafanuliwa kwenye jedwali hapo juu. Kazi zinazotarajiwa kutekelewa ni katika maeneo ya:
  - Kufanya kazi za awali (Preliminaries)
  - Kujenga Msingi wa Jengo (Sub structure)
  - Kunyanyua Jengo (Super Structure)
  - Kuezeka (Roof Structure and covering)
  - Kazi ya kuweka milango na Madirisha
  - Umaliziaji (finishing) wa jengo
  - Rangi na mapambo (Painting and decoration)
  - Mfumo wa Maji Safi na Taka (Water Supply and Sewage System)
  - Landscaping (kumwaga zege, kerbstones, aprone, mtaro)Aidha, waombaji wote wanatakiwa kuonesha muda watakaoutumia katika kutekeleza na kukamilisha kazi za miradi walioiomba.
- vi. Katibu Tawala Mkoa ataingia mkataba na Fundi Mkuu mmoja, kikundi au Taasisi itakayokuwa na sifa na itakayokuwa imekidhi vigezo vyote vilivyotakiwa, ambapo fundi atawajibika kwa kazi zote kama zilivyoainishwa katika Kifungu Namba tano (V) hapo juu.
- vii. Maombi yatumwe kwa **Katibu Tawala Mkoa, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, S.L.P. 858, Iringa** kuanzia tarehe ya tangazo hili mpaka mwisho tarehe **12 April, 2023 saa 4.00 Asubuhi** na yakabidhiwe kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni aliyeko Jengo la Uhasibu, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Iringa.

viii. Ni lazima waombaji wawe na sifa na wazingatie maelekezo yafuatayo:-

- (a) Mwombaji aoneshe uzoefu wake katika kazi za ujenzi kwa kipindi cha kuanzia tarehe 1 Januari 2023 hadi sasa, kwa kuonesha sehemu alizofanya kazi kwenye majengo ya Serikali, muda uliotumika katika kutekeleza kazi hizo pamoja na gharama za kazi alizofanya na aambatanishe nakala ya mkataba alioingia na Taasisi husika.
- (b) Mwombaji awe na uwezo wa kusoma na kutafsiri ramani/michoro.
- (c) Mwombaji awe na vitendea kazi kulingana na zabuni atakayoomba na orodha ya vifaa hivyo iambatanishwe kwenye maombi.
- (d) Mwombaji apitishie maombi yake kwenye Serikali ya Uongozi wa kijiji au Mtaa anakoishi pia mwombaji awasilishe nakala ya kitambulisho cha mpiga kura/kitambulisho cha taifa/leseni ya udereva/kitambulisho cha Ujasirimali/TIN namba.
- (e) Waombaji wote wenye nia ya kushiriki katika ufunguzi wa zabuni wanakaribishwa kushiriki siku ya ufunguzi.
- (f) Maombi yoyote yatakayofika mara baada ya tarehe na muda wa mwisho wa ufunguzi hayatapokelewa wala kufunguliwa.
- (g) Ofisi haitalazimika kukubali au kukataa maombi yoyote kwa sababu zozote zilizo nje ya utaratibu uliopo kisheria.

ix. Siku ya kutembelea eneo la mradi ili kuweza kujaza makabrasha itakuwa tarehe 11/04/2023 (Jumanne). Waombaji wote wafike saa 4.00 kamili asubuhi katika Jengo la OFISI YA MKUU WA MKOA IRINGA ili kuonana na Mhandisi wa Mkoa ili kuwaonyesha eneo ulipo mradi. Gharama za kutembelea eneo la mradi kila mwombaji atajitegemea.

  
Elfas Luvanda

**KAIMU KATIBU TAWALA MKOA  
IRINGA.**